# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA NANE

**17 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA NANE – TAREHE 17 APRILI, 2025

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**96. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini idadi ya Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari waliohama kutoka Mkoa wa Mtwara Julai, 2023 - Juni, 2024 ni 318 na waliohamia ni 113.

**97. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Kibaga itajengwa kwa kiwango cha changarawe ili kuondoa kero ya watumiaji Tarime Mjini.

**98. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ushuru wa Kahawa unaotozwa na Halmashauri kwa Wakulima wa Mbozi na kote nchini unakokotolewa kwa bei ya Shambani au Sokoni.

**99. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka Watumishi katika Kituo cha Afya Kilakala Manispaa ya Temeke.

**WIZARA YA NISHATI:**

**100. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali imefikia wapi katika mradi wa kusambaza gesi ya kupikia majumbani Wilayani Kinondoni.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**101. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, kiasi gani cha fedha kimepelekwa kwenye ujenzi wa Chuo cha Ufundi Kayenze - Buchosa.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**102. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itatangaza Maporomoko ya Vinile yaliyopo Mvomero kuwa Kivutio cha Utalii.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**103. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuhakikisha kuwa maeneo ya Delta Kibiti yanafikiwa na mawasiliano ya Simu.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**104. MHESHIMIWA OMARI ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Ofisi ya NIDA katika Wilaya ya Micheweni.

**WIZARA YA MAJI:**

**105. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, kabla ya kuwa na mitambo ya uchimbaji wa Visima ya Serikali, gharama ya uchimbaji wa kisima ilikuwa kiasi gani ukilinganisha na gharama ya sasa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**17 APRILI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**